JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA JANUARI, 2019 NA MWELEKEO WA FEBRUARI, 2019

Dondoo za Januari, 2019

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya viashiria pamoja na mwenendo wa mvua kwa mwezi Januari, 2019 na mwelekeo wa viashiria matarajio ya mvua kwa mwezi Februari, 2019 nchini.

a) Maeneo mengi ya nchi yanayopata mvua mara moja kwa mwaka yameendelea kupata mvua za '*Msimu*' kama ilivyotarajiwa, aidha maeneo mengi ya nchi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka pia yamepata mvua za nje ya msimu katika kipindi cha mwezi Januari, 2019 na mtawanyiko wake ulikuwa wa kuridhisha.

b) Vipindi vya ukavu vinatarajiwa katika maeneo ya kati na magharibi mwa nchi hususani katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Februari, 2019, vipindi vya ukavu katika maeneo yaliyopo kusini mwa nchi vinatarajiwa katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2019. Aidha, katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2019 mvua zinatarajiwa hususani katika maeneo ya pwani ya kaskazini.

1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI, 2019.

Katika kipindi cha mwezi Januari, 2019, maeneo mengi ya nchi yanayopata msimu mmoja wa mvua yameendelea kupata mvua za '*Msimu*'. Maeneo yanayopa misimu miwili ya mvua (maeneo ya kanda ya ziwa, Nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini) yamepata mvua za nje ya msimu na mtawanyiko wake ulikuwa wa kuridhisha. Vipindi vifupi vya mvua kubwa viliripotiwa katika baadhi ya maeneo. Mnamo tarehe 5 Januari, 2019, kituo cha Mahenge kilipima kiwango cha mvua cha milimita 56.4 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kupimwa katika maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka katika kipindi chote cha mwezi. Aidha, tarehe 17 Januari, 2019 kituo cha KIA kilipima kiwango cha mvua cha milimita 63.3 ikiwa ni kiwango

cha juu zaidi kupimwa katika maeneo yanayopata mvua misimu miwili kwa mwaka.

Kwa ujumla mvua za *Msimu* ziliendelea vizuri katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka kama zilivyotarajiwa, katika kipindi chote cha mwezi Januari, 2019.

2.0 MWELEKEO KWA MWEZI FEBRUARI, 2019

2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari la juu ya wastani inatarajiwa katika eneo la Kitropiki la Bahari ya Pasifiki na maeneo ya kati Kusini mwa Bahari ya Hindi. Hali ya joto la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la Kaskazini Magharibi mwa Bahari ya Hindi karibu na pwani ya Somalia. Aidha, eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantic karibu na pwani ya Angola linatarajiwa kuwa na joto la wastani hadi chini ya wastani. Mashariki mwa Bahari ya Hindi pamoja na Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi kunatarajiwa kuwa na joto la juu ya wastani.

2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI FEBRUARI, 2019

Vipindi vya ukavu vinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi katikaa kipindi cha mwezi Februari, 2019.

2.2.1 Maeneo Yanayopata Misimu Miwili ya Mvua kwa Mwaka

Kwa ujumla kipindi cha mwezi Februari, 2019 maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa makavu.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Kwa ujumla vipindi vya ukavu vinatarajiwa katika maeneo mengi, aidha vipindi vya mvua vinatarajiwa kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari, 2019.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Vipindi vya ukavu kwa ujumla vinatarajiwa katika maeneo mengi.

Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): Kwa ujumla vipindi vya ukavu vinatarajiwa katika maeneo mengi.

2.2.2 Maeneo Yanayopata Msimu Mmoja wa Mvua kwa Mwaka

Mvua katika maeneo haya zinaendelea kama ilivyotarajiwa, ingawa vipindi vya ukavu vinatarajiwa kujitokeza.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vya ukavu vinatarajiwa katika maeneo mengi hususan katika wiki ya kwanza na

ya pili ya mwezi Februari, 2019, vikifuatiwa na vipindi kadhaa vya mvua katika wiki mbili zilizosalia.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Vipindi vya ukavu vinatarajiwa katika maeneo mengi hususan katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Februari, 2019 vikifuatiwa na vipindi kadhaa vya mvua katika baadhi ya maeneo katika wiki mbili zilizosalia.

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa na Mbeya): Vipindi vya mvua kiasi vinatarajiwa kuendelea kwa baadhi ya maeneo katika kipindi cha wiki ya kwanza ya mwezi Februari, 2019 ikifuatiwa na vipindi vya ukavu katika baadhi ya maeneo kuanzia wiki ya pili ya mwezi Februari, 2019.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Kwa ujumla hali ya mvua, inatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Februari, 2019. Aidha vipindi vya ukavu vinatarajiwa katika wiki mbili zilizosalia.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Kwa ujumla hali ya mvua, inatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Februari, 2019. Aidha vipindi vya ukavu vinatarajiwa katika wiki mbili zilizosalia.

Wakulima wanashauriwa kufuatilia tabiri za siku kumi na kuomba ushauri kwa maafisa ugani kilimo ili kujua hatua gani wachukue kutumia ipasavyo mvua hizi zinazotarajiwa.

Imetolewa na;
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.